



Australian Government


COVID-19 VACCINATION

Chanjo ya COVID-19 ni nini? Je, ni salama?



Ugonjwa wa Virusi vya Korona (COVID-19) unasababishwa na **virusi** ambavyo huathiri watu wengi kote ulimwenguni.

Virusi vinaweza kusambaza kutoka kwa mtu mmoja kwenda mtu mwengine na kusababisha ugonjwa.




COVID-19 inaweza kusambaa:

- kwa rahisi
- kwa haraka.



Chanjo ya COVID-19 itatusaidia:

- kukaa salama
- kuishi kama tulivyozoea kabla ya COVID-19.



Chanjo ni matibabu ambayo:

- husaidia watu kupambana na virusi wakati ikiwa inawasiliana navyo
- inaweza kuzuia watu kuumwa sana kutokana na virusi.



Chanjo ya COVID-19 inafunza mwili wako jinsi ya kupambana na COVID-19.



Kuchanjwa ni pale unapopigwa na sindano ya chanjo. Hii inafanywa na sindano.



Kuchanjwa kwa COVID-19 ni bure kwa kila mtu nchini Australia hata kama huna kadi ya Medicare.



Unaweza kuchagua kupata chanjo.



Lakini si lazima ikiwa huitaki chanjo.

Je, chanjo ya COVID-19 ni salama?



Wanasayansi kote ulimwenguni wametengeneza chanjo tofauti za COVID-19.



Nchini Australia, **Utawala wa Bidhaa ya Matibabu (yani, Therapeutic Goods Administration (TGA))** huidhinisha chanjo kabla ya hazijaweza kutumiwa.



TGA ni sehemu ya Idara ya Afya ya Serikali ya Australia.



TGA huidhinisha tu chanjo ambazo:

- ni salama
- zinafanya kazi vizuri.



Baada ya kuwa imeidhinisha chanjo, TGA:

- inatunza orodha ya chanjo ambazo iliziidhinisha



- inafuatilia jinsi chanjo zinavyofanya kazi katika jamii.



Hii inajumuisha:

- jinsi chanjo inavyofanya kazi vizuri
- jinsi gani chanjo inavyokuwa salama.



TGA imeshaidhinisha chanjo mbili za COVID-19 nchini Australia. Hizi zinaitwa:

- chanjo ya Pfizer
- chanjo ya AstraZeneca.

Mambo ya kujua juu ya chanjo



Chanjo hazina COVID-19 yoyote ndani zao.

Hii inamaanisha kuwa chanjo haziwezi kukuambukiza COVID-19.



Baada chanjo yako bado kuna uwezekano unaweza kupata ugonjwa wa COVID-19 kutoka watu wengine.

Hii inamaanisha kila mtu bado anahitaji kusaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19.



Bado wewe unatakiwa:

- kuweka umbali angalau wa mita 1.5 kutoka watu wengine



- kunawa mikono yako mara kwa mara kwa kutumia sabuni na maji



- tumia sanitiza wakati usipoweza kutumia sabuni



- vaa maski (barakoa) kama jimbo au eneo lako linasema unahitaji kuvaa



- kaa nyumbani ikiwa unajisikia vibaya



- pata kipimo ikiwa una dalili zozote za COVID-19.



Hauwezi kufuatiliwa kwa kupata chanjo ya COVID-19.

Chanjo za COVID-19 hazina teknolojia ndogo sana ndani yake, kama:

- programu
- microchips.



Chanjo ya COVID-19 haitasababisha uwe **mgumbe**.

Ikitokea ukawa mgumbe, huwezi:

- kuzaa mtoto
- kuwa mjamzito.



Chanjo za COVID-19 hazitabadilisha DNA yako.

DNA yako ni habari maalum juu yako ambayo imo kila seli katika mwili wako.



Ikiwa huna hakika kama unaweza kupata chanjo, uzungumzia na daktari wako kwanza.

Habari zaidi



Unaweza kutembelea tovuti ya Idara ya Afya kwa www.health.gov.au/covid19-vaccines-languages ili kupata maelezo zaidi juu ya chanjo katika lugha yako.



Unweza kupigia simu kwa Simu ya Msaada ya Virusi vya Korona ya Kitaifa kwenye **1800 020 080**.

Ikiwa unahitaji habari katika lugha mbali ya Kiingereza, pigia simu Huduma ya Utafsiri na Ukalimani kwenye **131 450**.